


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI NA MADINI



TARATIBU ZA USAFIRISHAJI NA UINGIZAJI WA
MADINI TANZANIA

1. Nani mmiliki wa madini ndani ya ardhi ya Tanzania?

Kwa mujibu wa Kifungu Namba 5 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 madini yaliyopo juu, chini au ndani ya ardhi ya Tanzania Bara ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, inatakiwa kupata kibali kutoka mamlaka husika ya Serikali ili kuweza kutafiti, kuchimba na kufanya biashara ya madini nchini.

2. Ni sheria ipi inayoruhusu mtu kumiliki au kuwa na madini?

Kifungu Namba 6 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinakataza mtu yeyote kutafiti au kuchimba madini bila kuwa na leseni halali ya madini inayotolewa chini ya sheria hiyo.

Kwa mujibu wa Kifungu Namba 7 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, leseni za madini zifuatazo hutolewa kwa waombaji: leseni ya utafutaji madini (PL), leseni ya utafutaji wa madini ya vito (GPL), leseni ya zuio (RL), leseni maalum ya uchimbaji mkubwa (SML), leseni ya uchimbaji mkubwa (ML), leseni ya uchimbaji mdogo (PML), leseni ya uchenjuaji mbale (*processing licence*), leseni ya kuyeyusha madini (*smelting licence*) na leseni ya kusafisha madini (*refining licence*).



Tanzanite

Pia, Vifungu Namba 76 na 83 vya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 vinaruhusu wamiliki wa leseni kubwa na ndogo za biashara ya madini kununua, kumiliki au kuuza madini. Vilevile, Kanuni ya 16 na 17 za Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 zinaruhusu mgeni kununua au kupata madini kutoka kwa mchimbaji au mfanyabiashara wa madini mwenye leseni halali, au kununua madini kutoka kwenye Maonesho ya Biashara ya Vito nchini na kuyasafirisha nje ya nchi baada ya kutimiza masharti ya kisheria.

3. Nani mwenye haki ya kufanya biashara au kusafirisha madini nje ya nchi?

Wamiliki wenye leseni za madini zifuatazo wana haki ya kufanya biashara au kuuza madini nje ya nchi: leseni maalum ya uchimbaji mkubwa (SML), leseni ya uchimbaji mkubwa (ML), leseni ya uchimbaji mdogo (PML), leseni ya uchenjuaji mbale (*processing licence*), leseni ya kuyeyusha madini (*smelting licence*) na leseni ya kusafisha madini (*refining licence*).

Aidha, Vifungu Namba 76 na 83 vya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 vinawaruhusu wamiliki wenye leseni kubwa ya biashara ya madini (*dealer licence holders*) na leseni ndogo ya biashara ya madini (*broker licence holders*) kununua, kumiliki na kuuza madini.

Pia, Kanuni ya 16 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inaruhusu mgeni kusafirisha nje ya nchi madini aliyoyapata kutoka kwa mchimbaji au mfanyabiashara wa madini mwenye leseni halali kwa kuomba kibali maalum kutoka kwa Kamishna wa Madini, baada ya kulipa ada na mrabaha stahiki kwa madini hayo.

Vilevile, Kanuni ya 17 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inaruhusu mgeni kusafirisha nje ya nchi madini aliyoyapata kutoka kwenye Maonesho ya Biashara ya Vito nchini, baada ya kulipa ada na mrabaha stahiki kwa madini hayo.

Mgeni mwenye Viza ya Kitalii (*Tourist Visa*) pia anaruhusiwa kusafirisha madini nje ya nchi, kwa mujibu wa Kanuni ya 16(2) ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010. Ada maalum (Dola za Marekani 200) hutozwa pale ambapo mgeni huyo atataka kusafirisha madini yenye thamani isiyo zidi Dola za Marekani 1,000. Iwapo thamani ya madini husika inazidi Dola za Marekani 1,000 mgeni huyo atatakiwa kulipa ada ya Dola za Marekani 2,000.



Tomalini ya kijani



Angalizo:

- i. Kanuni ya 16 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inampa fursa mgeni mwenye Viza ya Kitalii kusafirisha madini nje ya nchi si zaidi ya mara mbili kwa mwaka.
- ii. Wamiliki wa leseni ndogo za biashara ya madini (*broker licence holders*) hawaruhusiwi kusafirisha madini nje ya nchi.

4. Vibali gani vinahitajika ili kuweza kusafirisha madini nje ya nchi?


Madini au sampuli za madini zinaweza tu kusafirishwa nje ya nchi na mmiliki mwenye leseni ya uchimbaji madini au mfanyabiashara mkubwa wa madini mwenye leseni halali. Vibali vifuatavyo vinahitajika wakati wa kusafirisha madini au sampuli za madini kutoka Tanzania:

- a. Kibali cha Kusafirisha (*Export Permit*):** Kibali cha Kusafirisha madini au sampuli za madini kinatolewa na Kamishna wa Madini kikionesha, pamoja na mambo mengine, jina la mwenye leseni, namba ya leseni, aina ya madini, uzito wa madini, thamani ya madini yanayosafirishwa, uthibitisho wa malipo ya mrabaha, tarehe ya kutolewa kibali, ukomo wa kibali cha kusafirisha na jina la Afisa aliyetoa kibali.
- b. Kibali cha Kusafirisha Madini Yaliyonunuliwa kwenye Maonesho ya Biashara ya Vito (*Export Permit for Minerals from Gem Trade Fair*):** Kanuni Namba 17 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inaruhusu wageni kusafirisha madini waliyonunua kwenye Maonesho ya Biashara ya Vito nchini baada ya kulipa ada na mrabaha stahiki. Katika hali hii, Kibali Maalum cha Kusafirisha Madini nje ya nchi hutolewa na Kamishna wa Madini kwa mujibu wa Fomu MTF 18.
- c. Cheti cha Kuthibitisha Uasilia wa Madini ya Tanzanite (*Certificate of Origin for Tanzanite Minerals*):** Kanuni Namba 18(1) ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inataka kila Kibali cha Kusafirisha Madini ya Tanzanite kiambatane na Cheti cha Kuthibitisha Uasilia kilichotolewa na afisa aliyeruhusiwa. Cheti cha Uasilia kinaonesha, pamoja na mambo mengine, jina la mwenye leseni, uzito wa madini na thamani ya madini ya Tanzanite yanayosafirishwa, tarehe ya kutolewa cheti, na jina la afisa aliyetoa cheti hicho
- d. Cheti cha Mauzo ya Almasi (*Tanzania Kimberley Process Certificate*):** Kwa upande wa almasi, kila Kibali cha Kusafirisha almasi lazima kiambatane na Cheti cha Mauzo ya Almasi kinachotolewa na afisa aliyeruhusiwa kutoka Ofisi ya Kimberley Process iliyopo chini ya Kamishna wa Madini.
- e. Kibali Maalum cha Kusafirisha Madini Nje ya Nchi (*Special Export Permit*):** Kanuni ya 16 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inamtaka mgeni anayetaka kusafirisha madini aliyoyapata kutoka kwa mchimbaji aliyeruhusiwa au mfanyabiashara wa madini

kuomba Kibali Maalum cha Kusafirisha madini hayo nje ya nchi kutoka kwa Kamishna wa Madini.

Hata hivyo, mgeni mwenye Viza ya Kitalii (*Tourist Visa*) hutozwa ada maalum (Dola za Marekani 200) pale ambapo atataka kusafirisha madini yenye thamani isiyo zidi Dola za Marekani 1,000. Iwapo thamani ya madini inazidi Dola za Marekani 1,000 mgeni huyo atatakiwa kulipa ada kamili (Dola za Marekani 2,000). Kanuni hiyo pia inampa fursa mwenye Viza ya Kitalii kusafirisha madini nje ya nchi si zaidi ya mara mbili kwa mwaka.


Katika hali yoyote, uthibitisho wa malipo ya mrabaha kwa madini yanayosafirishwa nje ya nchi ni lazima utolewe na msafirishaji kwa Maafisa wa Forodha na Wakaguzi wa TMAA kabla ya kuruhusiwa kusafirisha mzigo huo nje ya nchi.



Almasi

Muhimu:

- i. Kila kibali cha kusafirisha madini au sampuli za madini nje ya nchi ni lazima kiambatane na ankara halisi (invoice) na Stakabadhi ya Malipo ya Serikali (ERV) kwa ajili ya ada ya maombi ya kibali cha kusafirisha madini nje ya nchi na malipo ya mrabaha wa madini husika.
- ii. Kanuni ya 5(4) ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inataka kila kibali cha kusafirisha madini au sampuli za madini kuachwa na mwenye leseni kwa Afisa wa Serikali (Forodha au Postamasta) katika kituo cha kutoka nje ya nchi (exit point). Kibali hicho kinatakiwa kurejeshwa kwa afisa aliyekitoa (Issuing Officer).



5. Vibali gani vinahitajika wakati wa kuingiza madini nchini?

Kanuni ya 4 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inataka uingizaji wa madini au sampuli za madini ndani ya nchi ufanyike baada ya kupata kibali cha kuingiza madini nchini (Import Permit) kutoka kwa Kamishna wa Madini.

Kibali hicho, pamoja na mambo mengine, huonesha jina la mwingizaji, aina ya madini, uzito na thamani ya madini au sampuli za madini zinazoingizwa, mahali yanapoingilia nchini, mahali yanapokwenda, njia ya usafirishaji, madhumuni ya kuingiza madini au sampuli hizo nchini, ada ya uingizaji, tarehe ya kutolewa kibali na jina la afisa aliyetoa kibali. Aidha, Kanuni ya 6(9) ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inataka kibali cha kuingiza madini nchini kiwasilishwe kwa mkusanyaji wa forodha ambaye atakiwasilisha mara moja kwa Kamishna wa Madini.

Muhimu:


- i. **Usafirishaji wa Madini na Sampuli za Madini Zilizolingizwa Nchini (*re-export*):** Kanuni ya 7 ya Kanuni za Uchimbaji (Biashara ya Madini) za Mwaka 2010 inaweka wazi kuwa madini yaliyoingizwa nchini (*imported minerals*) hayataruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi na mwingizaji hadi hapo atakapopata kibali cha kuyasafirisha (*permit to re-export*). Kibali hicho hutolewa na Kamishna wa Madini baada ya kujiridhisha kuwa, kiasi cha madini yanayotakiwa kusafirishwa nje ya nchi kinalingana na madini yaliyoingizwa nchini. Vinginevyo, maelezo ya madini yaliyopungua au kuzidi ni lazima yawekwe bayana.
- ii. **Madini Yanayosafirishwa Kupitia Nchini (*Minerals on Transit*):** Madini yanayosafirishwa kupitia nchini yanashughulikiwa chini ya Kanuni za Forodha zinazohusu bidhaa zinazopita (*transit goods*) ambapo madini hukaguliwa yanapofika mpakani (*entry point*) kwa kuhakiki vifurushi au makasha yenye madini husika. Kwa upande wa madini yenye mionzi, ni lazima kufanyiwa ukaguzi na Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) kwa kushirikiana na Kamishna wa Madini kama inavyofafanuliwa kwenye Kifungu Namba 108 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni za Uchimbaji (Madini ya Mionzi) za Mwaka 2010. Mizigo na lakiri hukaguliwa upya katika vituo vya kutokea (*exit points*) ili kuhakikisha kuwa hakuna udanganyifu uliotokea wakati wa usafirishaji wa madini na sampuli husika ndani ya nchi.

Ni muhimu kusesitiza hapa kuwa Kifungu Namba 101(5) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinampa Kamishna wa Madini au afisa yeyote aliyeruhusiwa, nguvu za kuingia na kupekua sehemu yoyote, gari, meli au ndege bila kuhitajika kuwa na Hati ya Upekuzi endapo kuna sababu za kimsingi kuamini kuwa kuna kosa limefanyika chini ya sheria.

Kwa hatua hii, Kamishna wa Madini na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania wana mamlaka ya kukagua madini yanayopitishwa nchini kama kuna sababu ya kufanya hivyo.

6. Je, kuna adhabu gani kwa makosa yanayohusiana na biashara haramu na utoroshaji wa madini?

Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinakataza mtu yeyote zaidi ya mmiliki halali wa leseni ya madini, kumiliki, kusafirisha au kuuza madini bila kuwa na kibali cha kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria. Kifungu cha 18(3) kinakataza mtu yeyote kusafirisha nje ya nchi madini au sampuli za madini bila kuwa na leseni ya madini, kibali cha kusafirisha madini nje ya nchi na uthibitisho wa malipo ya mrabaha.



Dhahabu



Kwa mujibu wa Kifungu cha 18(4) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, mtu yeyote atakayekiuka Sheria kuhusiana na umiliki na biashara ya madini akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichozidi Shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitatu, au adhabu zote mbili. Kwa kampuni adhabu iliyopo kwa mujibu wa Sheria kwa kosa hilo ni kulipa faini isiyo zidi Shilingi milioni hamsini.

Kifungu cha 6(4) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, kinampa mamlaka Kamishna wa Madini kutaifisha madini yaliyopatikana kinyume cha Sheria, pamoja na vifaa vilivyotumika kuzalisha madini hayo.

7. Je, Kamishna wa Madini na Afisa aliyeidhinishwa wana mamlaka gani mahsusi ya kisheria katika kushughulikia biashara haramu ya madini?

- a. Kuingia na kufanya upekuzi kwenye eneo, ofisi, jengo, gari, au vyombo vya usafiri wa anga na majini bila kuhitajika kuwa na Hati ya Upekuzi endapo atahisi kuwepo kwa uwezekano wa ukiukwaji wa Sheria – Kifungu 101(5) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.
- b. Kuchukua sampuli za udongo, mawe, makinikia, au madini kwa lengo la kufanya uchunguzi wa kimaabara – Kifungu 101(1)(e) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

- c. Kuchukua taarifa na vielelezo vitakavyoonekana kuhitajika katika usimamizi wa Sheria – Kifungu 101(1)(g) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.
- d. Kumkamata mtuhumiwa yeyote, kwa msaada wa Jeshi la Polisi
- e. Kutaifisha madini yaliyopatikana kinyume cha Sheria – Kifungu 6(4) cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

8. Je, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania una jukumu gani katika kukabiliana na biashara haramu na utoroshaji wa madini nchini?

Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (Tanzania Minerals Audit Agency - TMAA) ulianzishwa tarehe 2 Novemba, 2009 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura ya 245. Tamko la Waziri la kuanzisha Wakala lilichapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 362 la tarehe 6 Novemba, 2009. Aidha, Kifungu cha 4 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinaipa mamlaka ya



Mkaguzi wa TMAA akichukua sampuli ya makinikia ya shaba

kisheria TMAA kukagua shughuli za uchimbaji na biashara ya madini nchini.

Lengo la kuanzishwa kwa Wakala ni kuhakikisha Serikali inapata mapato stahili kutoka kwenye shughuli za uzalishaji na biashara ya madini nchini kupitia usimamizi na ukaguzi makini wa shughuli hizo.

Pamoja na majukumu mengine, TMAA imepewa dhamana ya kuzuia biashara haramu ya madini na utoroshaji wa madini

nje. Kazi hii hufanyika kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Jeshi la Polisi na Idara ya Uhamiaji.

Katika kutekeleza jukumu hilo kikamilifu, Wakala umeanzisha Madawati ya Ukaguzi wa Madini kwenye viwanja vyote vya kimataifa vya ndege nchini.

9. Je, ada zipi zinazotozwa wakati wa kusafirisha nje na kuingiza madini nchini?

Aina ya Kibali	Kusafirisha Nje	Kuingiza nchini
Kibali cha kusafirisha madini au sampuli za madini	USD 100	USD 300
Kibali maalum cha kusafirisha madini kwa wageni (kwa madini yenye thamani inayozidi USD 1,000)	USD 2,000	-
Kibali maalum cha kusafirisha madini kwa wageni wenye Viza ya Kitalii (<i>Tourist Visa</i>) – kwa madini yenye thamani isiyoziidi USD 1,000.	USD 200	-
Kibali maalum cha kusafirisha madini yaliyonunuliwa kwenye mnada (<i>Gem Trade Fair</i>)	USD 200	USD 200

10. Viwango gani vya Mrabaha hutozwa kwenye mauzo ya madini?

Kifungu cha 87 cha Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kinaainisha viwango vifuatavyo vinavyotumika kukokotoa mrabaha kwenye thamani halisi ya madini yaliyouzwa:

Aina ya Madini	Kiwango cha Mrabaha
Urani, madini ya vito (ghafi) na almasi (ghafi)	5%
Madini ya metali (shaba, dhahabu, fedha na metali za kundi la platinum)	4%
Madini ya vito na almasi iliyokatwa	1%
Madini mengine: madini ya ujenzi, chumvi, madini ya viwandani na mengineyo	3%

MAWASILIANO YA HARAKA

Jina	Wadhifa	Kituo cha Kazi	Namba ya Simu	Namba ya Simu ya kiganjani
Eng. Ally B. Samaje	Kaimu Kamishna wa Madini	Dar es Salaam	+255 22 211 7156 +255 22 211 7159	+255 782 664 085
Eng. Paul Masanja	Mtendaji Mkuu - TMAA	Dar es Salaam	+255 22 260 1819	+255 754 297 408
Eng. Edwin Ngonyani	Mkaguzi Mkuu wa Madini	Dar es Salaam	+255 22 211 5696	+255 754 466 108
Eng. Benjamin Mchwampaka	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Kaskazini	Arusha	+255 27 254 4079	+255 786 366 968
Mr. Alex Magayane	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Mashariki	Dar es Salaam	+255 22 215 0243	+255 784 310 576
Mr. Salim S. Salim	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Ziwa Victoria	Mwanza	+255 28 250 0066	+255 787 533 986
Eng. David Mulabwa	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Magharibi	Mpanda	+255 25 282 0194	+255 784 337 212
Mr. Humphrey Mmbando	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Kati Magharibi	Shinyanga	+255 28 276 3282	+255 754 576 503
Mr. Manase Z. Mbasha	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Kati	Singida	+255 26 250 2075	+255 784 645 227
Mr. Aloyce Tesha	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Kusini	Mtwara	+255 23 233 3552	+255 754 291 062
Eng. John Shija	Kamishna Msaidizi wa Madini – Kanda ya Kusini Magharibi	Mbeya	+255 25 250 2921	+255 788 735 563
Mr. Shubi Byabato	Kamishna Msaidizi wa Uchumi na Biashara ya Madini	Dar es Salaam	+255 22 211 7156 +255 22 211 7159	+255 767 360 666
Eng. Dominic Rwekaza	Mkurugenzi wa Uthamini wa Madini na Huduma za Maabara - TMAA	Dar es Salaam	+255 22 260 1819	+255 754 951 551
Mr. George Kaseza	Meneja wa Uthamini wa Madini - TMAA	Dar es Salaam	+255 22 260 1819	+255 767 498 869
Mr. Omar Sige	Mkuu wa Dawati la Mrabaha - TMAA	Dar es Salaam	+255 22 260 1819	+255 767 555 739

1. Leseni Kubwa ya Biashara ya Madini (*Dealer Licence*)


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE MINING ACT, 2010
Made Under Section 73
DEALER LICENCE

FORM MTF. 6

Licence is hereby granted to (Full name) _____
of (Full address) _____

to buy, sell or otherwise deal in minerals _____
(type of minerals) for the period of _____
months(s) from the date of issue at the following premises: _____

This licence is issued subject to the following terms and conditions:-

Dated at _____ this _____ day of _____ 20____

ZONAL MINES OFFICER, _____

Specimen

Note:
1. This licence must be displayed at the place of business specified herein.
2. The licensee shall be liable for the due and full payment of royalties and other prescribed fees in respect of all minerals bought, sold, received or exported by him.

2. Kibali cha Kusafirisha Madini Nje ya Nchi (*Export Permit*):


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

FORM MTF. 2

THE MINING ACT, 2010
THE MINING (MINERAL TRADING) REGULATIONS, 2010
(Made Under Regulation 8)

EXPORT PERMIT FOR MINERALS AND SAMPLES OF MINERALS

EP/MTN No. 00000546

Permission is hereby granted to (full name) _____
holder of Licence No. _____ of (full address) _____
on behalf of (name and address of
owner of minerals) _____

To export _____ package(s) containing (variety and net weight
of minerals) _____

_____ by (state means of transmission
from Tanzania and post office or place at which the minerals are to be
exported) _____

I hereby certify that the payment (provisional payment) in lieu of royalty, due from the
licensed dealer in respect of these minerals has been received.

This permit is valid for a period of _____ days from the date hereof.
This permit is issued subject to (the following condition(s):-

Dated at _____ this _____ day of _____, 20____

Authorized Officer

3. Cheti cha Kuthibitisha Uasilia wa Madini ya Tanzanite (Certificate of Origin for Tanzanite Minerals):


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE MINING ACT, 2010
THE MINING (MINERAL TRADING) REGULATIONS, 2010
(Made Under Regulation 23)

CERTIFICATE OF ORIGIN FOR TANZANITE MINERALS

TZ. No. 00000501

Permission is hereby granted to (full name) _____

holder of Licence No./Passport No. [For a non-resident] _____

of [full address] _____

containing tanzanite minerals weighing _____

_____ grams /carats

and valued at US Dollar _____

_____ in Tanzania

The tanzanite minerals in the shipment have been handled in accordance with the provisions of the Mining Laws of Tanzania.

Issued at _____ on _____ day of _____, 20____

COMMISSIONER FOR MINERALS

GP-DSM

4. Cheti cha Mauzo ya Almasi (Kimberly Process Certificate)

FORM DTF-2

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
THE MINING ACT,
[CAP 123]
THE MINING (DIAMOND TRADING) REGULATIONS, 2003
Made under Regulation 9

CERTIFICATE OF EXPORTATION FOR ROUGH DIAMONDS
(KIMBERLEY PROCESS CERTIFICATE)

Permission is hereby granted to [full name] _____ of [full address] _____
holder of Licence No. _____ to export _____ parcel(s)
containing rough diamonds weighing _____ carats and value at US dollars (USD) _____
mined in _____ [country where extracted].

HS Classification is shown hereunder:

HS Codes	Weight (carat)	Value (US\$)
7102.10		
7102.21		
7102.31		
Total		

The parcel(s) will be exported by _____ [state means of transmission from Tanzania
and place or post office at which the minerals are to be exported] to [name and address of importer/consignee].

This permit is valid for a period of 30 days from the date hereof.

This permit is issued subject to the following condition(s):-

**The rough diamonds in the shipment have been handled in accordance with the provisions of the
Kimberley Process International Certificate Scheme for rough diamonds.**

Date at _____ this _____ day of _____ 20____

COMMISSIONER FOR MINERALS

Certificate No. TZ N^o 00001421

Import Confirmation

Country of destination		
Identification of importer (Name and Address)		
HS Codes	Weight (carat)	Value (US\$)
7102.10		
7102.21		
7102.31		
Total		

Date of receipt by Importing Authority

Authentication by Importing Authority

To be returned to the Commissioner for Minerals,
Ministry of Energy and Minerals,
P. O. Box 2000, Dar es Salaam,
United Republic of Tanzania.

5. Cheti cha Uthamini wa Madini ya Vito (Gemstones Valuation Certificate)

 THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA MINISTRY OF ENERGY AND MINERALS DIAMOND & GEMSTONES VALUATION UNIT-TANSORT	
Certificate No: TAN./GV	00000133
Issued to:	
GEMSTONES VALUATION CERTIFICATE (Single/Parcel*)	
Following Grading and evaluation of parcel ID No: the outlined below are the findings:	
Weight:	Other Comments:
Grade:	
High:	
Medium:	
Low:	
Colour/Clarity Treatment:	
PROVISIONAL/FINAL VALUE*	
US\$:	
Value in words:	
Given this day of	
Signature of Authorised person	Signature of Authorised person
Dar Head Office:	Antwerp Office:
Ministry of Energy and Minerals	TANSORT-Tanzania Embassy
P. O. Box 2000	Lange Herentalse Straat 62-70
Dar es Salaam, Tanzania.	2018 Antwerpen, Belgium.
	
GP-Dsm	

**KAMISHNA WA MADINI
WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Barabara ya Samora
S.L.P. 2000, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 213 7142
Nukushi: +255 22 212 3688
Barua pepe: info@mem.go.tz
Tovuti: www.mem.go.tz



WAKALA WA UKAGUZI WA MADINI TANZANIA

Ofisi Kuu

Kitalu Na. 1129, Barabara ya Chole, Masaki
S.L.P. 23400, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 260 1819
Nukushi: +255 22 260 1326
Barua pepe: info@tmaa.go.tz
Tovuti: www.tmaa.go.tz



Tawi la Mwanza

Ghorofa ya 5, Jengo la PPF Plaza,
Kitalu Na. 17/2 & 18, Barabara ya Kenyatta,
S.L.P. 362, MWANZA
Simu: +255 28 2506052
Nukushi: +255 28 2506051
Barua pepe: info@tmaa.go.tz